WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA (TAWA)

HOTUBA YA KAIMU KAMISHNA WA UHIFADHI- TAWA, MABULA MISUNGWI NYANDA, KATIKA KIKAO KAZI NA WAHARIRI WA VYOMBO VYA HABARI UNAOFANYIKA KATIKA PORI LA AKIBA PANDE, TAREHE 10 SEPTEMBA, 2022 JIJINI DAR ES SALAAM

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TAWA - Meja. Gen. (Mstaafu) Hamis Semfuko,

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, Bw. Deodatus Balile,

Manaibu Kamishna wa Uhifadhi,

Wahariri wa vyombo vya habari,

Maafisa na Askari wa Uhifadhi,

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Itifaki imezingatiwa.

1. UTANGULIZI

Ndugu Wahariri

Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwepo mahali hapa katika siku ya leo. Kwa heshima kubwa napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana kwa kukubali mwaliko wetu wa kuhudhuria kikao kazi hiki muhimu.

Lengo la kikao kazi hiki ni kuendelea kuimarisha ushirikiano mzuri kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na vyombo vya habari. Sote tunafahamu kuhusu umuhimu na nafasi ya vyombo vya habari katika kuendeleza uhifadhi wa rasilimali ya wanyamapori na shughuli za utalii nchini na hivyo kuchangia katika juhudi za kukuza uchumi na usatwi wa wananchi kwa ujumla.

Ndugu Wahariri

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (*Tanzania Wildlife Management Authority - TAWA*) ilianzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha **8** cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori **Na. 5** ya Mwaka 2009 na kutangazwa kwa amri (*Orde*r) ya Serikali iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali **Na. 135** la tarehe 09 Mei 2014, pamoja na marekebisho yaliyochapishwa katika gazeti la Serikali **Na. 20** la tarehe 23 Januari 2015. TAWA ilianza kazi rasmi tarehe 1 Julai 2016 kwa kuchukua majukumu ya kiutendaji ya Idara ya Wanyamapori kuhusu usimamizi wa rasilimali ya wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa na Hifadhi ya Ngorongoro.

1.1 Majukumu ya TAWA

Ndugu Wahariri

TAWA ina jukumu la Kuhifadhi, kusimamia na kuendeleza rasilimali ya wanyamapori nje ya Hifadhi za Taifa na Eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kutekeleza yafuatayo: -

i. Kusimamia Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu;

ii. Kusimamia himasheria na kuzuia ujangili wa wanyamapori;
iii. Ulinzi na usimamizi shoroba za wanyamapori, maeneo ya mtawanyiko ardhioevu, maeneo ya wazi yenye wanyamapori kwa kushirikiana na wadau na taasisi nyingine za uhifadhi;
iv. Uangalizi na usimamizi wa wanyamapori katika ardhi za vijiji, Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori-WMAs, bustani za wanyamapori (Zoos), mashamba na ranchi za wanyamapori;
v. Kutatua migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kushirikiana na wadau na taasisi nyingine za uhifadhi;
vi. Kushirikiana na taasisi nyingine katika masuala yanayohusu uhifadhi wa wanyamapori;
vii. Kushirikiana na sekta binafsi na wananchi kuainisha fursa za uwekezaji zitokanazo na rasilimali ya wanyamapori;
viii. Kutoa, kuhuisha, kusitisha au kufuta vibali na leseni za matumizi ya wanyamapori;
ix. Kutoa elimu kwa wadau kuhusu umuhimu wa wanyamapori;
x. Kushirikisha wadau katika kuhifadhi na kunufaika na raslimali ya wanyamapori;
xi. Kushiriki katika utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kitaifa;
xii. Kuzingatia masuala ya utawala bora katika usimamizi wa wanyamapori; na
xiii. Kujenga na kuimarisha uwezo wa Mamlaka katika usimamizi wa wanyamapori.

Aidha, kupitia Tangazo la Serikali (GN) Na. 631 la tarehe 14 Agosti 2020, TAWA ilikasimiwa jukumu la kusimamia maeneo ya Malikale ya Kilwa Kisiwani, Songomnara, Sanje ya Kati na Majoma na pamoja na Kunduchi. Mamlaka ilipokea jukumu hilo na kuanza kuendeleza maeneo hayo kwa kuboresha miundombinu pamoja na kuwezesha usimamizi wa shughuli za kila siku.

1.2 Maeneo yanayosimamiwa na TAWA

Ndugu Wahariri

TAWA inasimamia maeneo yenye ukubwa wa jumla ya kilomita za mraba **136,287.06** yanayojumuisha Mapori ya Akiba **27** (yenye ukubwa wa kilomita za mraba **97,187.06**) na Mapori Tengefu **25** (yenye ukubwa wa kilomita za mraba **39,100**). Aidha, TAWA ni mwangalizi wa shughuli za usimamizi wa wanyamapori kwenye maeneo **21** ya Jumuiya

ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA) zenye ukubwa wa jumla ya kilometa za mraba **28,223.13**. Vilevile, TAWA ni msimamizi wa shughuli za ufugaji wa wanyamapori zinazohusisha mashamba (**6**), Bustani za Wanyamapori (**29**)**,** Ranchi (**5**) na *Breeding sites* (**30**).

2. UTENDAJI WA MAMLAKA TANGU ILIPOANZISHWA

Ndugu Wahariri

Tangu kuanzishwa kwake, Mamlaka imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia malengo makuu matatu kama yalivyoainishwa katika Mpango Mkakati wake wa mwaka 2018/19-2022/23 ambao umehuishwa kwa ajili ya miaka mitano (2021/22 hadi 2025/26) ili kujumuisha vipaumbele vya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 na kuendana na vipaumbele na malengo makuu ya Serikali. Malengo Mikakati ya TAWA ni;

i. Kuimarisha ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori na maeneo ya Malikale,
ii. Uboreshaji wa huduma za utalii na kuwaridhisha wateja,
iii. Kuongeza tija na ufanisi wa utendaji kazi.

2.1 Ulinzi wa Rasilimali ya Wanyamapori na Maeneo ya Malikale

2.1.1 *Kupunguza Kasi ya Ujangili*

Ndugu Wahariri

Kuimarika kwa ulinzi kulikochangiwa na kuongezeka kwa vitendea kazi, morali ya watumishi, na kuimarishwa kwa Kikosi cha Muitikio wa Haraka kumesababisha kupungua kwa matukio ya vifo vya tembo kutoka tembo **18** mwaka 2016/17 hadi Tembo watatu (**3)** mwaka 2020/21. Aidha, ujangili katika Pori la Akiba la Selous umepungua kutoka mizoga ya tembo saba (**7**) iliyoonekana kwa kipindi cha mwaka 2016/2017, ambapo kwa kipindi cha mwaka 2018/19 hadi 2020/21 hakuna mzoga wa tembo uliioonekana.

2.1.2 *Kudhibiti uvamizi wa mifugo kwenye maeneo ya hifadhi*

Ndugu Wahariri

Uvamizi wa mifugo katika maeneo ya hifadhi yanayosimamiwa na TAWA umeendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutokana na kuimarisha doria katika maeneo hayo. Kati ya mwaka 2016/17 na 2020/21 mifugo iliyokamatwa katika Mapori ya Akiba ilipungua kwa **asilimia 65.5** kutoka mifugo **56,708** mwaka **2016/17** hadi mifugo **19,554** kufikia mwaka **2020/21**.

2.1.3 Ushirikishaji jamii katika shughuli za uhifadhi

2.1.3.1 Uvuvi na ufugaji nyuki katika Hifadhi

Ndugu Wahariri

Katika kuimarisha mahusiano na wananchi kunufaika na Hifadhi katika maeneo yao, Mamlaka iliandaa mwongozo wa kusimamia shuguli za uvuvi na ufugaji nyuki katika maeneo hayo. Pamoja na kuimarisha mahusiano jumla ya **shilingi 870,671,385** zilikusanywa kutokana na shughuli za uvuvi (**Tsh**. **840,672,485**) na ufugaji nyuki (**Tsh**. **29,998,900**) katika Mapori ya Akiba ya Ugalla, Uwanda na Moyowosi na Pori Tengefu la Kilombero.

2.1.3.2 Kuwezesha miradi ya maendeleo kwa Jamii

Ndugu Wahariri

Katika mwaka 2021/22 Mamlaka ilikamilisha ujenzi wa soko la samaki katika wilaya ya Kiombero ambalo liligharimu milioni **66,000,000** ikiwa ni sehemu ya mchango wa TAWA jamii*.* Aidha, Mamlaka pia imeendelea kuchangia miradi mbalimbali ya jamii hususan inayolenga kwenye;

i. Elimu kupitia ujenzi wa madarasa, kununua madawati, ufadhili wa masomo,

ii. Afya kupitia ujenzi/ukarabati wa zahanati, kununua vifaa (baiskeli za walemavu),

iii. Maji kwa kuchimba visima, kuweka mabomba na kusambaza maji kwa wananchi, Maendeleo ya mifungo (kujenga majosho), na

iv. Mazingira kwa kutoa miche ya miti kwa wananchi waishio pembezoni mwa hifadhi.

2.2 Uboreshaji wa Huduma za Utalii na Kuwaridhisha Wateja

*2.2.1 **Kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa njia ya mnada***

Ndugu Wahariri

Mwaka 2019 Serikali ilianza utaratibu wa kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa njia ya mnada wa ki-elektroniki. Utaratibu huu umekuwa ukitumika na kuleta tija kwa mataifa mengine kama vile Zimbabwe, Zambia na Namibia. Njia hii ya kugawa vitalu vya uwindaji wa kitalii inatoa fursa kwa kampuni za uwindaji wa kitalii kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki. Aidha, utaratibu huu ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ya Chama Cha Mapinduzi inayolenga kuongeza idadi ya watalii hadi milioni tano na mapato hadi **US$ bilioni 6** ifikapo mwaka 2025.

Ugawaji wa vitalu vya uwindaji kwa njia ya mnada umekuwa na mafanikio yafuatayo: -

i. Kutoa fursa sawa kwa kampuni yoyote yenye sifa kupata kitalu cha uwindaji kwa njia ya mnada,
ii. Kuruhusu ushindani kwa kutoa nafasi ya wadau wengi kushiriki ikilinganishwa na utaratibu uliokuwa ukitumika awali;
iii. Kuongeza uwazi na uwajibikaji katika zoezi la ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii ili kuongeza ufanisi katika tasnia hii;
iv. Kuwezesha kugawiwa kwa vitalu vilivyorejeshwa kwa maudhui ya kutofaa katika uwindaji wa kitalii,
v. Ongezeko la ada ya vitalu kwa wastani wa asilimia **174** kama ifuatavyo: -
    - ✓ ada ya kitalu cha daraja la **I** kutoka dola za kimarekani **60,000** na kuuzwa kati ya dola za kimarekani **151,000** hadi **285,000**,
    - ✓ ada ya kitalu cha daraja la **II** kutoka dola za kimarekani **30,000** na kuuzwa kati ya dola za kimarekani **81,000** hadi **250,000**, na
    - ✓ ada ya kitalu cha daraja la **III** kutoka dola za kimarekani **18,000** na kuuzwa kati ya dola za kimarekani **31,000** hadi **255,000**.
vi. Kuongeza ushindani katika soko kwa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa kuzingatia ubora na daraja la kitalu.

Ndugu Wahariri

Mamlaka iliandaa mwongozo wa ugawaji wa vitalu vya uwindaji wa kitalii kwa njia ya mnada *Guidelines for Allocation of Hunting Blocks through Auctioning* pamoja na mfumo wa kielektroniki wa kufanikisha ugawaji wa vitalu hivyo. Tangu kuanza kwa ugawaji wa vitalu kwa njia ya mnada mwaka 2019, TAWA imeendesha jumla ya minada saba (**07**) ya vitalu vya uwindaji iliyohusisha vitalu **100** hadi kufikia Machi, 2022.

Katika awamu zote saba ambazo mnada ulifanyika, jumla ya vitalu **79** kati ya **100** viliuzwa kwa kiasi cha **Dola za Marekani 9,798,000**. Kiasi hicho cha fedha ni kubwa kuliko fedha ambayo ingepatikana kwa kuuza vitalu vyote **79** kwa njia ya kiutawala (administratively) ambapo zingepatikana fedha kiasi cha **Dola za Marekani 3,306,000** sawa na ongezeko la **asilimia 196.4**. Mamlaka itaendelea kufanya awamu kadhaa za minada ya kielektroniki hadi hapo vitalu vyote vilivyopangwa kufanyiwa minada hiyo vitakapomalizika.

2.2.2 Kuanzishwa kwa Uwekezaji Mahiri (Special Wildlife Investment Concession Areas-SWICA)

Ndugu Wahariri

Uwekezaji Mahiri kwenye maeneo ya wanyamapori yaliyohifadhiwa (Special Wildlife Investment Concession Areas **-** SWICA) ni aina mpya ya uwekezaji katika sekta ya utalii unaotekelezwa na TAWA. Uwekezaji huu umelenga kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka 5 wa TAWA (*Medium Term Strategic Plan*) wa mwaka 2020/21-2025/26, Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020. TAWA ilianza kutekeleza uwekezaji huu baada ya kujifunza kutoka kwa baadhi ya nchi zenye uzoefu ikiwemo; Afrika ya Kusini, Botswana, Msumbiji na Peru kwa kuwekeza kwenye baadhi ya vitalu kwa lengo la kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za utalii kwenye vitalu (*Wildlife Concession areas*) kwa kuzingatia kuwa ni aina ya utalii unaolenga zaidi watu matajiri (*High end customers*). Hadi sasa jumla ya maeneo saba yamegawiwa kwa wawekezaji watano na majadiliano kuhusu utaratibu za kutia saini mikataba kwa ajili ya uwekezaji kwa njia ya SWICA yanaendelea.

2.2.3 Kuimarika kwa Utalii wa Picha

Ndugu Wahariri

Kutokana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo utoaji wa chanjo ya UVIKO 19 na utangazaji wa utalii na kuvutia uwekezaji kupitia programu maalum ya “Tanzania - The Royal Tour” mwenendo wa utalii wa picha umeanza kuimarika. Katika

mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya watalii wa picha **158,108** walitembelea katika maeneo yanayosimamiwa na TAWA. Idadi hiyo ni ongezeko la **asilimia 76.2** ikilinganishwa na watalii wa picha **37,684** waliotembelea katika maeneo yanayosimamiwa na TAWA kwa mwaka 2020/21.

2.2.4 Mchango wa Shughuli za utalii kwa Jamii (benefit Sharing)

Ndugu Wahariri

Kutokana shughuli za utalii (utalii wa picha na uwindaji) Mamlaka imekuwa ikitoa gawio kwa Halmashauri za Wilaya, Vijiji na maeneo ya Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori-WMAs. Kati ya mwaka 2016/17 - 2021/22, Mamlaka imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 37.79** kwa wanufaika hao. Sambamba na hilo Kanuni za uwindaji wa kitalii zinaelekeza kampuni zilizokodishwa vitalu vya uwindaji kuchangia shughuli za maendeleo kwa walau dola za Marekani **5,000** kwa kila kitalu kwa mwaka.

2.2.5 Utalii katika Eneo la Malikale na Urithi wa Dunia Kilwa Kisiwani

Ndugu Wahariri

Eneo la Kilwa ni miongoni mwa fursa zilizoainishwa katika mkakati endelevu wa Mamlaka. Kwa kuwa eneo hili linapakana na Pori la Akiba Selous ambalo linatoa fursa za utalii wa wanyamapori, Mamlaka inaendelea kuweka mkazo katika kutangaza huduma hii mpya ya utalii wa maeneo ya malikale na fukwe. Hii ni pamoja kukamilisha ujenzi wa miundombinu wezeshi ya utalii ikiwemo jengo la mapokezi, hoteli na njia za waenda kwa miguu.

Aidha, Mamlaka imenunua boti ya kisasa ya utalii - ***Glass Bottom Boat*** ambayo ina uwezo wa kubeba abiria **30** kwa wakati mmoja kwa ajili ya shughuli za utalii katika maeneo ya Malikale la Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Aina hii ya kipekee ya boti inawezesha watalii kuona viumbe bahari wakiwa ndani ya boti hiyo. Sambamba boti ujenzi wa njia za waenda kwa miguu na ukarabati wa gati ulifanyika.

2.2.6 Kuboresha Miundombinu ya Utalii

Ndugu Wahariri

Katika kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na utalii yanaongezeka, Mamlaka imeboresha miundombinu katika maeneo ya utalii kwa kutumia fedha za bajeti ya maendeleo ya mwaka 2021/22 na fedha za Mradi wa ustawi wa Taifa na Mapambana dhidi ya UVIKO 19 ambapo miradi ifuatayo imetekelezwa: -

i. Ujenzi na ukarabati wa barabara yenye urefu wa kilometa **431.4**
ii. Kukamilika kwa ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Lake Natron na katika Pori la Akiba Maswa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Buturi umekamilika kwa **asilimia 50**,
iii. Ujenzi wa *Tourist Bandas* saba (**7**), *Campsites* sita (**6**), *picnic sites* nane (**8**) na *lounge* moja (**1**),
iv. Ujenzi wa malango na vituo vya kukusanyia mapato saba (**7**), na
v. Ujenzi wa njia ya waenda kwa miguu yenye urefu wa kilometa **1.2**.

2.3 Uboreshaji na Ufanisi wa Utendajikazi

*2.3.1 **Kuimarika kwa ukusanyaji wa Mapato***

Ndugu Wahariri

Vyanzo vikuu vya mapato kwa Mamlaka ni uwindaji wa kitalii na utalii wa picha. Kufuatia ya Mlipuko wa UVIKO 19, mapato kwa mwaka 2020/21 yalikuwa **Tsh. bilioni 25.75** sawa na **asilimia 47.46** ya makadirio ya lengo la kukusanya **Tsh. bilioni 54.25** katika mwaka husika. Ingawa jukumu la kukusanya mapato linatekelezwa na TRA, TAWA ilikadiria kukusanya jumla ya **Tsh. bilioni 61.1** katika wa mwaka fedha (2021/22) ambapo kwa mujibu wa mfumo wa MNRT Portal jumla ya **Tsh. bilioni 49.5** zilikusanywa kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato sawa na **asilimia 80 ya lengo**. Kwa ujumla mwenedo wa makusanyo ya mapato yatokanayo na utalii umeanza kuimarika.

*2.3.2 **Kutekeleza mfumo wa Jeshi Usu***

Ndugu Wahariri

TAWA kama zilivyo Taasisi nyingine za uhifadhi imeendelea kutekeleza mfumo wa jeshi, ambao ulizinduliwa rasmi mwezi Novemba, 2018 na aliyekuwa Makamu wa Rais ambaye kwa sasa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan. Jumla ya watumishi **1,407** kati ya **1,863** sawa na **asilimia 75.5** wamehitimu mafunzo. Lengo la mfumo huu ni kuongeza ufanisi katika ulinzi na usimamizi wa rasilimali za wanyamapori.

*2.3.3 **Kuweka Miundombinu Wezeshi***

Ndugu Wahariri

Mamlaka ilikamilisha ujenzi wa nyumba **14** za watumishi, kambi za askari (ranger post) **21**, ghala za silaha **16,** ofisi **06** na hosteli **1**. Aidha, Mmalaka imefanikisha ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari **115**, mahema **1,579**, boti **10,** gari/ Mtambo wa kuchimba visima mmoja (**1**), *Lowbed truck* moja (**1**) na *grader* **-1***.*

*2.3.4 **Utekelezaji wa miradi ya UVIKO 19***

Ndugu Wahariri

Katika fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, ***maarufu kama fedha za UVIKO 19***, TAWA iliidhinishiwa **TSh. Bilioni 12.9** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, ununuzi wa Mitambo, magari na vifaa vingine vya utalii na doria. Utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali ambapo ujenzi wa barabara kilometa **336.2** kati ya kilometa **463.5** sawa na **asilimia 72.5** umekamilika katika mapori ya Akiba Wami Mbiki, Kijereshi, Mkungunero, Lukwika Lumesule, Liparamba, Igombe na Rungwa. Aidha, ujenzi wa malango makubwa mawili (2) kati ya manne (4) katika Mapori ya Mkungunero na Swagaswaga umekamilika na malango mawili katika Mapori ya Wamimbiki na Kijereshi yapo katika hatua za umaliziaji (Finishing)**.** Vilevile, magari matatu (3) kati ya sita (6) yaliyoapngwa kununuliwa yalishapokelewa na magari matatu yaliyosalia yanatarajiwa kupokelewa Mwezi huu wa Septemba 2022 kutoka Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikalini (GPSA).

Ndugu Wahariri

Kupitia fedha hizi Mamlaka pia imenunua mtambo wa kulima barabara (grader) na gari la kuchimba visima ambalo litatumika kuchimba visima katika maeneo ya hifadhi na maeneo ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi. Aidha, Mamlaka imenunua boti nne (4) kwa ajili ya shughuli za utalii na doria, boti maalum kwa ajili ya shughuli za doria maeneo yenye ardhi chepechepe (amphibious boat) na boti moja ya kisasa (glass bottomed boat) yenye uwezo wa kubeba watu **60** kwa ajili ya shughuli za utalii kwenye eneo la kihistoria la Magofu ya Kilwa.

2.3.5 *Uandaaji wa Miongozo ya Kimkakati ya Usimamizi wa Mamlaka*

Ndugu Wahariri

Ili kuimarisha utendaji wa Mamlaka, jumla ya miongozo **15** ya Kimkakati ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka kwa ufanisi iliandaliwa na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi. Miongozo hiyo inalaenga kuimarisha utendajikazi katika maeneo ya rasilimali watu, usimamizi wa fedha, matumizi ya silaha, masuala ya TEHAMA na intelijensia, ugawaji wa vitalu, na ulinzi wa rasilimali ya wanyamapori ikiwa ni pamoja na miongozo ya utekelezaji wa mfumo wa Kijeshi kwa Jeshi la Uhifadhi (JU).

3. CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na:

3.1 Kutokuwa na utulivu wa kibiashara katika tasnia ya uwindaji wa kitalii

Ndugu Wahariri

Kumekuwa na ongezeko la kampeni za kupinga uwindaji wa kitalii ambazo zimezorotesha ustawi wa tasnia hii. Aidha Mlipuko wa UVIKO 19 umeongeza kuzorota kwa uwindaji.

3.2 Ongezeko la Matukio ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu

Ndugu Wahariri

Kwa ujumla, kuimarika kwa ulinzi wa rasilimali za wanyamapori kumesababisha kuongezeka sana kwa mtawanyiko wa wanyama katika maeneo mengi nchini, na hivyo kuongeza mwingiliano kati yao na binadamu. Kati ya mwaka 2016/17-2020/21 kulikuwa na matukio **6,472** ya wanyama wakali na waharibifu katika Wilaya **85** nchini ambayo yalisababisha watu kupoteza maisha, majeruhi, mifugo kuuwawa na mashamba kuharibiwa. Kwa mwaka 2020/21 pekee jumla ya siku watu za doria **12,491** zilitumika katika kukabiliana na matukio **1,706** katika wilaya **85** nchini.

3.3 Uvamizi maeneo yaliyohifadhiwa

Ndugu Wahariri

Wimbi la uvamizi kwa ajili ya shughuli za binadamu ikiwemo makazi, kilimo, uvuvi na mifugo katika maeneo yaliyohifadhiwa limeendelea kuwepo na kusababisha uharibifu wa bionuai. Aidha, uvamizi huo umesabisha migogoro mingi na uhasama usio wa lazima kati ya Mamlaka na wahusika na hata jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa. Mathalani, tatizo hili limekithiri sana katika Mapori Tengefu likiwemo Pori Tengefu la Kilombero ambalo ni chanzo kikuu cha maji cha mto Rufiji ambao maji yake yanatumika katika Bwawa la kuzalisha umeme la Mwl. Nyerere. Mamlaka inaishukuru Serikali Kwa marekebisho ya Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 ambayo imeweka utaratibu wa kushughulikia masuala ya mifugo inayokamatwa hifadhi kwa muda mfupi.

4. MWELEKEO WA MAMLAKA

Mwelekeo wa jumla wa Mamlaka umeainishwa kwa kina katika Mpango Mkakati wake wa miaka mitano (2021/22 hadi 2025/26) **ambao umeuhishwa ili kujumuisha vipaumbele vya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na kuendana na vipaumbele na malengo makuu ya Serikali.** Maeneo muhimu yatakayoendelea kutiliwa mkazo na Mamlaka katika miaka mitano ijayo (2021/22-205/26) ni pamoja na: -

i. ***Kuimarisha ulinzi wa rasilimali ya wanyampori na usimamizi wa maeneo ya malikale***

Ndugu Wahariri

Katika eneo hili, Mamlaka imelenga kudhibiti ujangili na uingizwaji wa mifugo katika mapori kwa **asilimia 90**, uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa shughuli za kilimo na makazi, ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwemo mtandao wa barabara. Vilevile Mamlaka itaendelea kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu, ulizi wa madhubuti wa wanyama waliohatarini kutoweka (vyura wa Kihansi, faru, flamingo, na mbwa mwitu) na upatikanaji wa vitendea kazi vya doria (magari, silaha, mahema, ndege & GPS) na ushirikishwaji wa jamii katika ulinzi na utatuzi wa migogoro.

ii. ***Kuimarisha shughuli za utalii***

Ndugu Wahariri

Mamlaka itaweka mazingira rafiki ya huduma za utalii wa picha na uwindaji, kujenga miundombinu ya utalii, barabara **kilomita 1,027**, mageti na vituo vya ukusanyaji wa mapato 22 na kiwanja cha ndege, kuongezeka kwa idadi ya watalii kufikia watalii wa picha **531,576** na watalii na uwindaji **1,000** pamoja na mapato kufikia **TSh. bilioni 103**. Vilevile Mamlaka itaongeza vitalu vyenye wawekezaji kutoka **asilimia 63** hadi **asilimia 100** kwa kugawa vitalu kwa njia ya mnada wa kielekronik (e-auction), SWICA, na njia nyingine. Aidha, Mamlaka itajikita katika kuimarisha hadhi, mvuto na msukumo wa biashara ya uwindaji wa kitalii iweze kushamiri na kuakisi hali ya soko la dunia. Mkazo utawekwa katika kutangaza vivutio vilivyopo katika uwindaji wa kitalii na utalii wa picha katika masoko makubwa ya biashara duniani, kubuni vivutio vipya vya utalii kuhamasisha ufugaji wa wanyamapori na kuibua fursa mpya za utalii.

iii. ***Kuongeza ufanisi wa utendajikazi***

Ndugu Wahariri

Mamlaka itaimarisha uwezo wa taasisi katika kutoa huduma. Watumishi watajengewa uwezo kwa kupewa mafunzo stahiki, vitendea kazi, miundombinu wezeshi na maslahi ya kiutumishi ikiwa ni pamoja na maboresho ya mishahara kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Mamlaka. Vilevile, Mamlaka itaweka mifumo madhubuti ya usimamizi wa fedha na kupima matokeo ya utendaji (*Financial and Performance management System*). Mamlaka pia itafungua kampuni ambayo itafanya biashara ikiwa ni njia ya kuongeza wigo wa mapato.

Ndugu Wahariri

iv. Mikakati mingine ya Mamlaka pamoja na: -

a. Kuendelea na utatuzi wa migogoro ya mipaka kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali yanayotokana na mapendekezo ya Kamati ya Mawaziri wa Kisekta**;**

b. Kuimarisha doria katika maeneo yanayokabiliwa na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna bora ya kuepuka madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu;

c. Kuendelea kuboresha miundombinu ya utalii kwa ajili ya kuendelea kuvutia watalii na wawekezaji.

5. HITIMISHO

Ndugu Wahariri

Mwisho, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kusema kuwa TAWA inatambua kwamba mafanikio ya uhifadhi hayawezi kupatikana bila kushirikiana na wadau wa habari mkiwemo ninyi wahariri. Ni matumaini yangu kuwa ushirikiano huu utakuwa endelevu na wenye manufaa kwa pande zote mbili. Aidha, Mamalaka inatatajia kupata ushirikiano stahiki kutoka kwa wahariri wa vyombo vya habari. Mwisho ila siyo kwa umuhimu, napenda kutumia nafasi hii kuwakaribisha sana kutembelea vivutio vinavyopatikana kwenye maeneo yanayosimamiwa na TAWA ili kwa pamoja tuendelee kuunga mkono jitihada za Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu za kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi yetu.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA